Mwongozo Wa Mwalimu

3

Mitazamo

Kutathmini na kukuza mitazamo

MVMM

Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

Mitazamo

Kutathmini na kukuza mitazamo

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo wa Mwalimu

Toleo la Tano

MVMM
Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

Mitazamo

Kutathmini na kukuza mitazamo

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo wa Mwalimu

Toleo la tano

Maandiko Yanayotumiwa Katika Kitabu Hiki Yametoka Kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kusambazwa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwa mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bila malipo. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo: *Attitudes, 5th edition*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, shuleni, katika huduma gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vile vile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, kitabu cha kuongoza mafunzo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.org na
www.iTeenChallenge.org

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 08-2023

Mitazamo

Kozi hii inaweka msingi kwenye mada inayotambulika ilhali ngumu sana kwa Wakristo wapya. Ni vipi haswa Wakristo ‘hufanya mawazo yao kuwa mapya’

1

Sura ya 1. Mitazamo katika maisha ya Mkristo Mpya

Mitazamo ni nini? Je, ninaitumia vipi katika maisha yangu ya kila siku? Ninaipata vipi?

2

Sura ya 2. Mchakato wa kujenga mitazamo mipya

Tunachanganua baadhi ya hatua mahususi za kuunda mitazamo mipya. Pia tunatazama jinsi Somo la Biblia linahusiana na uundaji wa mitazamo mipya na kuacha mitazamo ya kale.

3

Sura ya 3. Mtazamo unaofaa unaporekebishwa au kukosolewa

Je, tunapaswa kuitikaje tunapokashifiwa? Tulijibu swali hili kwa kuchunguza Mitazamo ya kibiblia tunayoweza kuitumia tunapoitikia Ukosoaji na urekebishaji. Sura hii pia inaangazia matatizo yanayohusu matumizi ya mitazamo mipya.

4

Sura ya 4. Mtazamo unaofaa kuwa nao unapomrekebisha mtu mwingine.

Katika sura hii tunajadili mtazamo wa kibiblia tunaopaswa kutumia tunapowakosoa wenzetu. Ni nani unayepaswa kumkosoa? Ni mbinu gani bora kabisa za kutumia kuwakosoa wengine? Ni mipaka ipi iliyowekwa na Biblia ya kuwakosoa wengine?

Yaliyomo Katika Mwongozo Huu Wa Mwalimu

Kitabu hiki kina sehemu nne. Kila sehemu imeanza kwa ukurasa wenye rangi ya njano, ambao ni ukurasa ulio na jina la mada.

1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo
2. Mwongozo Wa Mwanafunzi
3. Mwongozo Wa Somo
4. Mtihani Wa Mwanafunzi Na Cheti Cha Somo

Maelezo ya jinsi ya kutumia kila sehemu yanapatikana mara tu baada ya utangulizi wa ukurasa unaofuata.

Utangulizi

Hili ni somo moja katika mfululizo wa masomo ulioandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha Wakristo wapya. Tunaamini kwamba lipo hitaji kubwa sana siku hizi la kuwasaidia Wakristo wapya ili wahusishe mafundisho ya Kristo na maisha yao ya kila siku kwa vitendo. Mafundisho haya pia yanaweza kutumiwa vizuri sana kwa ajili ya huduma kwa vijana kanisani na watu wazima wanaotamani kufanya Ukristo kuwa sehemu ya maisha yao kila siku.

Kusudi kubwa la somo hili na mfululizo mzima wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* ni kuwatambulisha Wakristo wapya kwa maswali muhimu yanayohusu maisha. Hatujaribu kuwapa mafundisho yatakayokuwa ndiyo mwisho kuhusu mada husika.

Kamati ya Mtaala ya Huduma ya Teen Challenge Marekani, ina mpango wa kuendelea kupitia upya na kufanya marekebisho kwa masomo haya. Tunakaribisha mawazo yoyote au hoja za kutusaidia kuyaboresha.

Jinsi ya kutumia Mwongozo huu Wa Mwalimu

1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo

Kurasa za kwanza katika sehemu hii zinatoa mtazamo wa somo zima kwa ufupi.

Ukurasa unaofuata utakuwa ni nakala ya ***Orodha Ya Kazi Za Darasani***. Hii orodha inaonyesha wakati ambapo kila zoezi katika Mwongozo wa Somo linatakiwa kukamilishwa, na wakati kila chemsha bongo na mtihani zitatolewa. Kila mwanafunzi anapaswa kupewa habari stahiki kwa ajili ya ukurasa huo mwanzoni mwa kila somo. Kitabu hiki cha Mwongozo wa Somo tayari kina nakala isiyoandikwa chochote ya fomu hiyo, kwenye jalada la nyuma upande wa ndani.

Kitakachofuata ni mipango kwa ajili ya kufundishia kila somo. Hiyo yote ina kitu kinachoitwa Kweli Kuu ya Kibiblia pamoja na Mstari Mkuu. Hivyo vitu viwili vinaweza kutolewa mwanzoni mwa kipindi cha darasa. Pia vinasaidia kufanya mjadala ulenge yanayotakiwa kwa wakati wote.

Chini ya Kweli Kuu ya Kibiblia na Mstari Mkuu, kuna maelezo machache jinsi ya kufundisha somo lenyewe. Mara nyingi, marejeo yanaelekezwa kwa Mwongozo wa Mwanafunzi au kwa Zoezi linalopatikana katika Mwongozo wa Somo.

Kila somo humalizika kwa shughuli ya kufanya katika “Kufanyia Kazi Somo Maishani.” Umuhimu wa kipengele hiki hauelezeki. Wakristo wapya wanahitaji mwongozo ulio wazi kuhusu jinsi ya kuanza kufanyia kazi mafundisho haya katika maisha yao ya kila siku. Hakikisha kwamba una toa nafasi ya kutosha ili kuwasaidia wanafunzi wako kuanzisha shughuli hii.

Mwisho wa kila mpango wa kufundishia somo kuna orodha ya kazi za wanafunzi kufanya.

Mengi katika masomo haya yalikusudiwa kuwa na vipindi vitano vya darasa, kila kimoja kikidumu kwa saa moja. Kipindi cha mwisho darasani ni kwa ajili ya mtihani. Masomo yote 14 katika mfululizo huu yanaweza kukamilishwa katika kipindi cha miezi kati ya mitatu hadi

minne, kama darasa litakutana kwa siku tano katika wiki. Ikiwa unafanya darasa kwa saa moja tu kwa juma, unaweza kukamilisha somo moja kwa mwezi – na mfululizo wote kwa kama mwaka mmoja. Mengi katika haya masomo yanaweza kupanuliwa na kufundishwa kwa muda mrefu, au kwa madarasa zaidi.

2. Mwongozo Wa Mwanafunzi

Kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwanafunzi chaweza kutimiza makusudi mawili. Unaweza kutaka wanafunzi wasome kurasa husika katika kujiandaa kwa ajili ya somo linalofuata. Au, unaweza kuwataka wakisome baada ya wewe kufundisha somo, ili kufanya kama marudio na kuwa kama njia ya kusisitiza na kukazia kilichofundishwa darasani.

Tunakutia moyo uwaambie wanafunzi wajiandikie notsi darasani, hata ingawa utawapa Mwongozo Wa Mwanafunzi. Wanayojiandikia wenyewe pamoja na mazungumzo na mijadala darasani vitawasaidia sana kuelewa vizuri baadhi ya mada zinazoshughulikiwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

3. Mwongozo Wa Somo

Mazoezi yaliyo katika Mwongozo wa Somo yameandaliwa ili kumpa mwanafunzi kazi ya kufanya nje ya darasa. Baadhi ya kazi-mradi hizo zinasaidia kumwandaa mwanafunzi kwa ajili ya somo la darasa linalofuata.

Mengi ya mazoezi haya yamekusudiwa kuwasaidia wanafunzi wajikite ndani zaidi na kutazama baadhi ya maswala yanayojadiliwa darasani kwa kina. Lengo kuu la kazi hizo nyingi ni kuwaasaidia wanafunzi wagundue njia za kufanyia kazi hizo za kweli za Biblia katika maisha yao ya kila siku.

4. Mtihani Wa Mwanafunzi na Funguo la Majibu ya Mtihani

Mitihani hii imeandaliwa ili kutoa kipimo rahisi tu cha maendeleo ambayo kila mwanafunzi alipata katika uelewa wa kweli za Biblia zinazoshughulikiwa katika somo hili. Karatasi ya Majibu kwa ajili ya mtihani husika iko mara tu baada ya ukurasa wa mwisho wa ile nakala mfano ya mtihani wa mwanafunzi, katika Mwongozo huu wa Mwalimu.

5. Cheti Cha Somo

Cheti cha somo ni kwa ajili ya kuwatambua wale wanaomaliza kazi yote inayotakiwa kwa ajili ya somo hili na kufaulu mtihani. Mfano wa cheti hicho cha somo upo katika ukurasa wa mwisho wa kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwalimu. Cheti cha Kufuzu pia kinapatikana kwa wale wanafunzi wanaomaliza masomo yote 14 katika mfululizo huu wa *Mafunzo ya Vikundi Ya Maisha Mapya*. Pia, mfano upo katika kile kitabu kinachoitwa ***Kuwatambulisha waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***.

Jinsi Masomo Haya Yalivyotokea

Sulemani alisema, hakuna kitu kipya chini ya jua. Maneno hayo yanaweza kufaa hata kuhusu masomo haya. Mawazo yake mengi si mapya. Tunataka kutoa shukrani zetu maalum kwa Institute in Life Principles (Taasisi Ya Kanuni Za Maisha) kwa ushawishi mkubwa katika maisha ya watu waliotayarisha masomo haya. Masomo mengi yana alama za huduma hiyo ya Institue in Life Principles.

Nataka pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengi sana na maelfu ya Wakristo wapya ambao wametumia masomo haya katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita. Mawazo yao yamekuwa na mchango mkubwa sana katika maandalizi ya masomo haya.
Pia ninamshukuru sana Ndugu Don Wilkerson kwa kunipa nafasi ya kufanya kazi katika kituo cha huduma ya Teen Challenge pale Brooklyn, New York, tokea mwaka wa 1971 hadi 1975. Katika miaka hiyo ndipo matayarisho yalipoanza ya masomo haya yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*.

Toleo la tano la *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* lilitayarishwa kwa msaada wa kamati ya Mitaala ya huduma ya Teen Challenge Marekani. Natoa shukrani maalum kwa wote waliosaidia katika mapitio na marekebisho hayo.

Sera Kuhusu Kunakili Machapisho Haya

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi kinachohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* kinalindwa na Sheria za Haki Miliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali fulani, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kwenye mtandao kwa tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Dave Batty

Pendekezo Kuhusu Mpangilio Wa Kufundisha

Somo hili ni moja kati ya 14 katika mfululizo wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*. Masomo yote 14 yameorodheshwa hapa kama pendekezo la jinsi ya kuyafundisha. Mfuatano huu ulitayarishwa kwa ajili ya ufundishaji endelevu wa masomo haya. Tunaweza kuutazama kama picha ya gudurumu lenye vyuma kumi na vinne. Masomo haya hayategemei linalotangulia. Kila somo linasimama lenyewe. Basi, mwanafunzi anaweza kujiunga na madarasa wakati wowote na akaingia tu vizuri kwenye mfumo.

1. Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?
2. Kuitazama Biblia Kwa Haraka
3. Mtazamo
4. Majaribu
5. Maisha Ya Kikristo Yenye Mafanikio (ni pamoja na mafunzo juu ya huduma ya Roho Mtakatifu.)
6. Kukua kupitia kufeli
7. Matendo Ya Kikristo (Mahusiano Katika Kanisa La Mahali)
8. Utiifu kwa Mungu
9. Utiifu kwa Mwanadamu
10. Hasira na Haki za Kibinafsi
11. Jinsi Ya Kujifunza Biblia
12. Kujipenda na Kujikubali Mwenyewe
13. Mahusiano yako wewe Binafsi na Wengine
14. Nguvu Ya Kiroho na Mambo Yasio Ya Kawaida

Tazama kitabu kiitwacho, ***Kuwatanguliza waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***, ili kupata maelezo zaidi juu ya kufundisha masomo hayo.

Mipangilio ya Masomo

Kwa Mwalimu

Angalia ukurasa wa 4 wa Mwongozo wa Mwalimu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mipangilio hii ya masomo

Maelezo ya jumla ya kozi

1. Siku moja au mbili kabala ya kikao cha kwanza cha darasa, unaweza kutanguliza kozi kwa wanafunzi na kuwapa kazi za kwanza za kutenda. Ikiwezekana, wape Mwongozo Wa Somo siku moja au mbili kabla ya kuanza kufunza somo.

2. Katika ukurasa ufuatao kuna nakala ya *Orodha ya kazi darasani* ambayo inatoa tarehe ambayo kazi inapaswa kuwasilishwa. Waagize wanafunzi wajaze tarehe ifaayo wakitumia nakala tupu za *Orodha ya kazi za darasani* iliyoko nyuma ya Mwongozo Wa Somo.

3. Wajulishe wanafunzi ya kwamba wanapaswa kukamilisha zoezi la 1 kwenye mwongozo wa somo, *"Mitazamo ni nini?" kabla ya kipndi cha* darasa la kwanza. Unaweza pia kutoa maelezo mafupi ya zoezi 2, *"Kubadilisha Mitazamo Yako"*. Zoezi hili halihitajiki hadi kipindi cha darasa la pili. Waambie wasianze zoezi la 2 hadi mwisho wa darasa la kwanza.

   Waambie ikiwa hawaelewi kile wanachopaswa kutoa kama majibu wanaweza kuwaacha pengo. Wanaweza kumaliza sehemu hiyo ya Zoezi la 2 wakati wa kipindi cha darasa la kwanza au baadaye. Hata hivyo, wanapaswa kukamilisha maswali matatu ya kwanza kwenye mifano yote katika Zoezi la 2 kabla ya kipindi cha darasa la kwanza.

4. Wanafunzi wanaweza kupewa Mwongozo wa wanafunzi wakati wa kozi inayotangulzwa ikiandamana na mwongozo wa somo. Hata hivyo, unapofanya hivyo, waambie wanafunzi wakamilishe Zoezi la 1 mwongozo wa somo, kabla ya kusoma sura ya 1 katika mwongozo wa wanafunzi. Majibu ya baadhi ya maswali katika zoezi la 1 yako kwenye kurasa chache za kwanza kwenye mwongozo wa wanafunzi.

5. Somo la 1 & 2 linatoa fursa ya kuelezewa zaidi katika vikao viwili tofauti. Unaweza kusoma mipangilio ya somo ukaangalia ni ipi itakuwa bora kwa wanafunzi wako.

> Mtazamo wako uwe kama wangu, kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.
>
> Yesu Kristo
> Mathayo 20:28
> Tafsiri kutoka Biblia Habari Njema (SUV)

Orodha ya Kazi ya Ziada

Mada ya Somo: Mitazamo

Chemsha Bongo Mstari wa kumbukumbu Tarehe

1. Methali 10:17 (Biblia Habari Njema) Siku ya 2
2. Wagalatia 6:1 Siku ya 3
3. Mtazamo wa Kibiblia wa kuwa nao (ukurasa 16 katika mwongozo wa wanafunzi) Siku ya 3 or 4

Zoezi Tarehe ya Kuwasilisha

1. Siku 1
2. Siku 2 au 3
3. Siku 2
4. Siku 3 au 4
5. Siku 4 au 5
6. Siku 3
7. Siku 3
8. Siku 4
9. Siku ya 5 au ya kuchagua
10. Siku ya 5 au ya kuchagua

Mtihani Tarehe Siku 5

1 Somo la 1
Mitazamo ni nini?

1. Kweli Kuu ya Kibiblia

Ninahitaji kukuza mitazamo mipya kuitumia katika maisha yangu ya kila siku.

2. Mstari mkuu: Waefeso 4:23 (Biblia Habari Njema)

Mitazamo yako na mawazo yako yanapaswa kuwa yanabadilika yawe bora.

3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili

Sura ya 1 na ya 2 katika mwongozo wa wanafunzi zinatangamana na somo. Mwongozo wa somo zoezi 1, *"Mitazamo ni nini?"* unaambatana na somo.

4. Chaguo la vikao viwili vya darasa

Ikiwa ratiba yako itakukubalia, unaweza kupanga kutumia vikao viwili vya darasa kupitia somo la kwanza. Maswala makuu yanayopitiwa katika somo yanapasawa kupitiwa kando kando.

1. Mitazamo ni nini?
2. Je, mitazamo mipya hukuzwaje?

5. Zoezi la utangulizi wa somo: "Wasilisho la Mtazamo?" (Dakika 5-10)

Anza kikao cha darasa kwa onyesho la ana kwa ana linaloeleza baadhi ya mitazamo tunazoweza kuwa nayo katika matukio tofauti. Lengo kuu la onyesho hili ni kuchechemua hamu yao ili kuangazia kwa undani baadhi ya mitazamo inayoshawishi mienendo ya siku kwa siku.

Unaweza kufanya onyesho hili kwa mfumo wa *PowerPoint* au kuzichapa picha na kuwaonyesha wanafunzi.

Tengeneza onyesho tofauti kwa kila kauli iliyoorodheshwa hapa chini. Kuwa huru kuongeza kauli nyingine zinazoeleza mitazamo mingine. Jaribu kulinganisha mtindo, rangi ya mandharinyuma na kipengele kingine chochote cha Sanaa na mtazamo unaoonyeshwa.

Hizi hapa ni baadhi ya kauli za mitindo unazoweza kuzitumi katika onyesho.

1. Sheria hutungwa kukiukwa.
2. Jinsi viongozi wanavyopata ushawishi mkuu, ndivyo wanavyozidi kuwa wafisadi.
3. Matunda ya kuibwa ndio huwa matamu zaidi ya yote.
4. Cha msingi haswa ni kushinda mchezo.

5. Fedha hununua furaha ya kweli.
6. Upendo unaweza kutatua shida zote ulimwenguni.
7. Siasa huudhi.
8. Hatuna ubaguzi, sisi huwachukia wote.
9. Wazungu hujivinjari zaidi
10. Watu wakarimu huja kuwa matajiri.
11. Kwa nini tufanye kazi ilhali tunaweza kupata ushirika?
12. Chochote unachoweza kufanya, mimi naweza kukifanya hata bora zaidi.
13. Gharamia matakwa yako, omba mahitaji yako.

Tanguliza onyesho hili kwa wanafunzi kutumia maelezo mafupi kuhusu mitazamo mingi tofauti wanayokuwa nayo watu siku hizi. Waambie wafikirie mitazamo iliyoko nyuma ya kila kauli na picha katika onyesho.

Unapofanya onyesho hili, usichukue muda kujadili kila moja. Kusudi letu ni kuchechemua hamu yao kusoma mitazamo. Mwishoni mwa onyesho, ingia moja kwa moja katika hoja ifuatayo kwenye mwonozo wa somo. – *Mitazamo ni nini?*

6. Jadili Hoja A. Je, Mitazamo ni nini?
(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa 4-5
na Mwongozo wa Somo, Zoezi la 1

Jadili na wanafunzi baadhi ya fasili tofauti za neno "**mitazamo**". Wanafunzi wasome majibu yao ya swali la 1 katika Mwongozo wa Somo zoezi 1 "*Mitazamo ni nini*?" Andika majibu yao kwa ubao. Kwa wakati huu, kubali tu majibu yao hata kama sio sahihi.

Baada ya wao kutoa maelezo, basi eleza fasili tutakazozitumia kwa neno hili katika majadiliano ya darasa katika kozi hii. Unaweza kuwaambia watumie orodha ya fasili katika ukurasa wa 4 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

Mitazamo ni nini?

1. Mfumo wa kufikiria
2. Maoni
3. Jinsi unavyofikira
4. Tabia ya kufikiria
5. Mawazo niliyojifunza
6. Kauli ya kiakili kulingana na ukweli au jambo fulani

Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 4

1

7. Tofauti kati ya mitazamo na hisia
(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanfunzi, ukurasa 5)

Hakikisha kwamba wanafunzi wako wanaelewa tofauti kati ya mtazamo na hisia. Wanafunzi wasome majibu yao ya swali la 2 katoka Mwongozo wa Somo Zoezi la 1. Swali hili linawauliza waeleza tofauti kati ya mtazamo na hisia. Hoja hii pia imeangaziwa katika ukurasa wa 5 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

8. Mitazamo dhidi ya mitazamo mibaya (Dakika 3-5)

Baadhi ya wanaafunzi wako hutumia neno "mtazamo" kwa njia hii, "Ana mtazamo" ilhali wanachokirejelea ni kwamba "ana kiburi". Waeleze kikamilifu kwamba katika kozi hii hatutafsiri mtazamo kwa namna hiyo. Sote tuko na mitazamo, mingine mizuri na mingine mibaya. Waelekeze wanafunzi wako kwa maelezo yalitotolewa katika ukurasa wa 5 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi.

9. Yanayosemwa na maandiko katiko Wafilipi 2:1-11 kuhusu mitazamo
(Dakika 4-6) Mwongozo wa Somo, Zoezi 1

Wanafunzi wasome majibu yao ya swali la 3 kwenywe Mwongozo wa Somo Zoezi la 1. **Soma Wafilipi 2:1-11 (haswa mst. 5). Je, Andiko hili linakuambia nini juu ya mitazamo?**

Sisitiza hoja kwamba tunapaswa kuwa na mitazamo sawia na yale aliyokuwa nayo Kristo – tazama Wafilipi 2:5.

10. Jadili Warumi 12:2 kuhusu Mitazamo (Dakika 4-6)

Wanafunzi wafungue Biblia na kusoma Warumi 12:2 kutoka kwa tafsiri tofauti na nukuu za kisasa. Kwa ufupi jadili yanayosemwa katika andiko hili kuhusu mitazamo ya Mkristo mpya.

11. Zoezi la vikundi vidogo « kuchukua au kuacha » (Dakika 15-25)

Kwa zoezi hili, gawa darasa kwa vikundi vya wanafunzi 4-5.
(Ikiwa darasa ni dodo, ligawe katika vikundi viwili)

a. Tanguliza zoezi hili kwa kuelezea kwamba Mungu anatuambia katika Biblia tuache aina fulani ya mitazamo na tabia. Mungu pia anatuambia tuchukue aina nyingine ya tabia na mitazamo.

b. Agiza kikundi kimoja (au zaidi) kuosma Wakolosai 3:5-15.
Kikundi kingine nacho kisome Waefeso 4:17-32.

c. Kila kikundi kitengeneze orodha mbili.

Orodha #1 Nini cha kuacha au kuangamiza kabisa.

Orodha #2 ni nini cha kuchukua na kukuza katika maisha yetu.

Wape makaratasi mawili makubwa na kalamu za kuandika. Waandike orodha zao kwenye makaratasi. (Uwape dakika 8-12 kumaliza zoezi hili.)

d. Baada ya wao kumaliza zoezi hili, tundika orodha zote mbele ya darasa. Kisha mwanafunzi mmoja katika kila kikundi atoe maelezo ya matokeo yao. (dakika 5-10)

12. Kutoka sura ya 2 katika mwongozo wa mwanafunzi. Jadili Hoja A. Je, ni katika sehemu gani za maisha yangu ninahitaji kukuza mitazamo mpya? (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa 7-8

Sehemu iliyosalia katika mwongozo wa somo la leo linaangazia maswali yanayoibuka katika sura ya 2 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

Iwapo una muda, unaweza kujadili swali la 4 na 5 katika Mwongozo wa Somo Zoezi la 1. Lakini, iwapo hakuna muda, ruka na uingie moja kwa moja katika swali la 6 Zoezi 1.

(4) *Unapataje mitazamo?*
(Je, unaundaje au unatengenezaje mitazamo?)

(5) Je, Unatumiaje mitazamo yako katika maisha yako ya kila siku?

(6) Je, ni maeneo gani ya maisha yako ambayo unataka kukuza mitazamo mipay?

Wanafunzi watambue ni mitazamo ipi muhimu zaidi kwa mkristo mpya kubadilika. Watumie orodha kutoka waefeso 4:17-32 na Wakolosai 3:5-15. Wanaweza pia kutumia majibu waliyotoa katika zoezi la 1, swali la 6. Unaweza kuwauliza wanafunzi wachache kueleza kwa nini mitazamo hii (waliyotaja) ni muhimu kwa mkristo mpya.

13. Mitazamo miwili mikuu kuhusu Ukosoaji

Baada ya wanafunzi kutoa maoni kuhusu mitazamo iliyo muhimu zaidi kwa mkristo mpya ambayo anapaswa kukuza, ongeza mitazamo miwili ifuatayo iwapo haipo katika orodha.

• Mtazamo wangu ninapokosolewa (au ninapokashifiwa)

• Mtazamo wangu ninapomkosoa mtu ambaye ninafikiria amefanya mabaya

Waeleze kwamba tutachukua somo moja kwa kila mojawapo ya mitazamo. Pia unaweza kuwaambia watazame orodha ya mitazamo katika ukurasa 7 ya Mwongozo wa wanafunzi chini ya hoja A. *"Je, ni katika sehemu gani za maisha yangu ninahitaji kukuza mitazamo mipya?"*

14. Jadili Hoja B. Nianze wapi katika kukuza mitazamo mipya? (Dakika 5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa 8-9

Kwa sehemu iliyosalia katika somo hili, tutaangazia jinsi tunavyoweza kubadili mitazamo yetu. Kwa ufupi, unaweza kujadili hoja katika ukurasa wa 8-9 katika Mwongozo wa Mwanafunzi, Sura ya 2, hoja B, *"Nianze wapi katika kukuza mitazamo mipya?"* Unaweza kutumia mifano iliyotolewa katika Mwongozo wa Mwanafunzi kueleza mambo matano yaliyoorodheshwa katika sehemu hii ya somo (mtazamo wa mtu kwa kazi).

1

15. Jadili Hoja C. Ni njia zipi zitanisaidia kukuza mitazamo mipya? (Dakika 15-25) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 10-13

Tumia muda wa kutosha kujadili Hoja C, *"Ni njia zipi zitanisaidia kukuza mitazamo mipya?"* Jaribu kutoa maelezo kwa kila mojawapo ya mbinu nne zilizotolewa katika mwongozo wa wanafunzi.

16. Kutendea somo kazi maishani (Dakika 10-20)

Wanafunzi wafungue Sura ya 2, *"Kubadilisha Mitazamo Yako,"* katika Mwongozo wa Somo.

A. Moja kwa moja, kila mwanafunzi ajibu swali la 1-5. Swali la 3: *"Ni maeneo gani mawili tofauti ambapo tunaweza kuanza kubadilisha mitazamo yetu?"* linatokana na maswala katika Hoja C *"Ninapataje mitazamo?"* katika Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 5-6. Kuna orodha ya angaa majibu 4 hapo.

B. Kisha waweke kwenye vikundi (viwili au vitatu) na wajadili majibu yao ya swali la 4 katika Mwongozo wa Somo Zoezi la 2. *«Fikiria juu ya mistari tofauti ya Biblia tuliyoiangalia darasani leo (somo la kwanza). Je, ni kifungu kipi cha Biblia kuhusu mitazamo kimekusaidia zaidi leo? (Andika hapa.)»* Uwaamuru kuwaeleza wenzao kwa nini kifungu hicho kimekuwa cha manufaa.

C. Kama wangependelea, basi unaweza kuwaruhusu kuonyeshana majibu ya swali la 5, *"Je, ni mtazamo gani mmoja katika maisha yako unaotaka kubadilisha?"*

D. Kisha kila moja amuombe mwenzake ili Mungu aweze kumsaidia abadili mtazamo wake.

E. Kama bado kuna muda, wanafunzi wajibu swali la 6 katika Mwongozo wa Somo Zoezi la 2 kabla ya kutoka darasani. *"Orodhesha jambo moja unaloweza kufanya katika saa 24 zijazo ili kusaidia kubadilisha mtazamo huu (zaidi ya kuomba juu yake)."*

17. Kazi za somo

A. Wape wanafunzi Mwongozo wa Mwanafunzi ikiwa bado haukuwa umefanya hivyo. Ikiwa unatumia mwongozo wa somo kutumia vikao 4 tu kufunza kozi hii, wanafunzi wasome Sura ya 3 katika Mwongozo wa Mwanafunzi kujitayaraisha kwa majadiliano ya darasa lifuatalo. Iwapo umeugawa mwongozo huu wa kwanza kwa vipindi viwili vya darasa, unaweza kuaagiza wanafunzi wasome tena sura ya 1 na ya 2 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

B. Sahihisha Zoezi la 1 kwenye Mwongozo wa Somo *"Mitazamo ni nini?"*

C. Iwapo unafuata mfumo wa kufunza kozi hii kwa vipindi vine (4) vya darasa, wakumbushe wanafunzi kwamba Mwongozo wa Somo Zoezi la 3, *"Uzoefu Wangu wa Zamani wa Kurekebishwa au Kukosolewa"* ni lazima ikamilishwe kabla ya darasa lifuatalo la *Mitazamo.*

18. Tathmini ya somo

Tafadhali orodhesha maoni yako ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu gani ziliokuwa bora zaidi?
Ni sehemu gani zilizokuwa ngumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni nini kilichokuwa cha manufaa kwa wanafunzi wako?

Somo la 2
Kurekebishwa au kukosolewa

2

1. Kweli Kuu ya Kibiblia

Ninapaswa kujua na kutumia mtazamo wa kibiblia ninaporekebishwa au kukosolewa.

2. Mstari Mkuu: Methali 10:17 (Biblia Habari Njema (SUV)

Akubaliye kurudiwa huwa katika njia ya uzima; Bali yeye aachaye maonyo hukosa.

3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili

Sura ya 3 katika mwongozo wa mwanafunzi unaambatana na somo hili. Mazoezi yafuatayo kutoka kwa mwongozo wa somo pia unaambatana na somo hili.

Zoezi la 3 *Uzoefu Wangu wa Zamani wa Kurekebishwa au Kukosolewa*

Zoezi la 4 *Kuangalia Mara ya Pili Marekebisho na Ukosoaji wa Wakati Uliopita*

Zoezi la 5 *Kutumia Mtazamo Wangu Mpya Wakati Mtu Ananisahihisha*

4. Zoezi la utangulizi wa somo: "Toa alama kwa Ukosoaji" (Dakika 5)

Simulia kisa katika maisha yako ambapo mtu alikurekebisha au kukukosoa. Eleza kwa hakika jinsi ulivyofanya. Kisha uwaulize wanafunzi wakadiri sehemu zifuatazo za simulizi lako.

(1) Kadiri uzito wa dhambi, kosa au upungufu wa yule aliyerekebishwa au kukosolewa. Tumia kipimo cha 1-10 ambapo 1 ni jambo dogo na 10 jambo kuu.

(2) Kadiri ubora wa kazi aliyoifanya yule aliyekurekebisha au kukukosoa. Tumia kipimo cha 1-10 ambapo 1 ni kazi duni sana na 10 kazi nzuri sana (yenye wema, maarifa na usikivu).

(3) Kadiri jinsi unavyodhania aliitikia yule aliyekuwa anarekebishwa au kukosolewa. Mpe alama katika ya 1 na 10. Alama 1 ikiwa unafikiria aliitikia vibaya sana na 10 kumaanisha alifanya vyema kabisa kwa ukomavu.

Zoezi hili ni la masihara tu na lenye kusudi la kusisimua fikira zao kuhusu maswala tunayotaka kuyajadili katika darasa la leo. Epukana na majadiliano marefu kwa sasa. Una uhuru wa kurejelea maelezo haya wakati wowote katika darasa la leo.

5. Chaguo la vikao viwili vya darasa

Kuna maarifa mengi yanayoambatana na somo hili. Uwezekano wa majadiliano marefu unaweza kukurai kupitia somo hili kwa vipindi viiwili badal ya kimoja.

6. Hapo mwanzoni, taja kwa ufupi jinsi kipindi cha darasa la leo kinavyohusiana na Somo la tatu.

Waambie wanafunzi wahifadhi maswali na maoni yao kuhusu *jinsi ya kumkosoa mwingine* hadi somo la tatu. Leo tutaangazia mtazamo wangu ninaporekebishwa. Taja pia kwamba mtazamo huu unaweza kutumika ninapokosolewa.

7. Toa mifano binafsi ya kurekebishwa au kukosolewa (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwananfunzi, ukurasa 14 na Mwongozo wa Somon Zoezi 3

Unaweza kuwa na wanafunzi wachache, waeleze kwenye darasa mojawapo wa mifano waliyoiandika kwa Mwongozo wa Somo Zoezi la 3, *"Uzoefu Wangu wa Zamani wa Kurekebishwa au Kukosolewa"*. Jaribu kuepuka majadiliano ya kina kuhusu nani alikuwa mwenye haki na na alikuwa mkosefu. Uwakubalie kutoa mifano yao na maoni jinsi inavyostahiki kwa mazungumzo ya leo.

Ikiwa wanafunzi hawataki kushiriki kwa mifano yao, wape mifano toka maishani mwako, ama ya wanafunzi wa hapo awali. Unaweza kutaja kwa ufupi maoni mengine kutoka kwa Sura ya 3, Hoja ya A, "*Ni kwa nini watu hunionea?*" Tazama ukurasa la 14 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

8. Uzinzi wa Daudi na Bath-Sheba (Dakika 5-15)

Tumia kisa cha nabii Nathani akimkaripia Mfalme Daudi kuhusu dhambi zake dhidi ya Bathsheba na Uria kutoka kitabu cha 2 Samweli: 11:1 - 12:25. Huu ni mfano mwafaka kutoka kwa Biblia ya jinsi mtu anavyoitikia anapokosolewa. Unaweza kumpa nafasi mwanafunzi mmoja atoe muhtasari wa hadithi hii katika darasa. Tazama kwa makini 2 Samweli 12:1-14 ambapo kuna mazungumzo kati ya Mfalme Daudi na nabii Nathani. Jadili mwitiko wa Daudi pale Nathani alipomwambia dhambi yake. Pia unaweza kusoma Zaburi 51 iliyoandikwa baada ya Nathani kumwendea Daudi.

Ingekuwa mufti kuzungumza kwa ufupi kuhusu hadithi hii ya Biblia katika darasa. Wanafunzi wasome 2 Samweli 11 na 12 na Zaburi 51 kabla ya kipindi cha darasa lifuatalo. Zaburi 51 inaonyesha vyema mtazamo wa Daudi baada ya kukosolewa. Unaweza pia kuwauliza waeleze mpango ambao Nathani aliutumia kumkosoa Daudi. Hilo linaweza kutumika katika somo la tatu (3) tunapojadiliana jinsi ya kuwakosoa wengine.

9. Mifano ya Biblia ya watu walivyoitikia kukosolewa kutokana na mtazamo mbaya (Dakika 5-10)

Unweza kutaja kuwa kuna mifano mingi katika Biblia ya watu walioitikia kukosolewa kwa mtazamo mbaya.

1. Adamu na Hawa – Hawakukubali kwamba walitenda dhambi katika shamba la Edeni. (Mwanzo 3:8-13)

2. Kaini – alikata kukosolewa na Mungu kuhusu sadaka yake. (Mwanzo 4:1-12)

3. Herode – hakutaka kufuata Ukosoaji wa Yoane Mbatizaji kuhusu ndoa yake kwa Herodia. (Mathayo 14:1-12)

4. Mfalme Kijana tajiri – Hakutaka kuacha mali yake. (Mathayo 19:16-24)

5. Wasadukayo na Wafarisayo – Walikataa Ukosoaji wa Yesu. (Mathayo 12:9-14)

2

10. Jadili Hoja B. Je, ni mtazamo gani wa kibiblia unaofaa wakati unarekebishwa au kukosolewa? (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 14-23

Rejelea taaena fasili ya mtazamo (ukurasa wa 4 katika Mwongozo wa Mwanafunzi). Eleza kwamba mtazamo ni *mfumo wa kufikiria.* Mseto huu wa fikira utatuongoza kutathmini jinsi ya kuitikia katika hali fulani.

Tanguliza kwa mtazamo mpya wa kibiblia wa kutumika wakati tunapokosolewa. Tazama hoja B katika ukurasa wa 14-23 kwenye mwongozo wa wanafunzi. Kwa upesi, pitia kila wazo linalounda mtazamo huo mpya wa kutumia pale unaporekebishwa au kukosolewa. Wanafunzi warejelee mawazo haya katika ukurasa wa 15 kwenye mwongozo wa mwanafunzi au safu ya 1 kwenye chati ukurasa wa 28-29.

Baadaye waruhusu wanafunzi wasome na kujadiliana mistari ya maandiko inayowiana na kila wazo. Katika Mwongozo wa Mwanafunzi hii imeorodheshwa katika ukurasa wa 15 na katika mstari wa sita wa mchoro ulio katika kurasa 28-29.

Mtazamo wa kibiblia unaofaa wakati wewe unasahihishwa au unakosolewa

1. Ninarekebishwa (au kukosolewa). Mithali 10:17
2. Nitasikiliza kwa makini. Yakobo 1:19
3. Ninashukuru kwamba ananirekebisha. 1 Wathesalonike 5:18
4. Nilikosea. Mithali 28:13
5. Ninawezaje kuzuia jambo hili baya kutokea tena? Mithali 15:31-32

Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi Ukurasa wa 15

Unaweza kutengeza chapa kubwa la chati kuhusu mtazamo huu wa kibiblia katika ukurasa wa 28-29 katika Mwongozo wa Mwanafunzi. Tundika chati hii kwa ukuta unakoweza kurejelea kwa urahisi unapoendelea na somo la leo, na sehemu iliyosalia ya kozi (isipokuwa wakati unapotahini mtazamo huu).

Kwa sasa, usionyeshe kwenye chati taarifa nyingine zote zinazoambatana na mtazamo huu katika ukurasa wa 28-29 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

11. Elezea mtazamo huu mpya (Dakika 5-10)

Toa mifano 2 au 3 ya jinsi watu wameutumia mtazamo huu na yaliyotendeka. Tumia mifano ya maisha yako binafsi au ya wanafunzi wa awali waliomaliza

Mwongozo wa Somo Zoezi la 5, *"Kutumia Mtazamo Wangu Mpya Wakati Mtu Ananisahihisha"*.

Jaribu kuonyesha jinsi kila hatua ilivyotumika au kutotumika na matokeo ya matumizi ya mtazamo huu. Unaweza pia kurejelea mfano wa nabii Nathani akimkosoa Mfalme Daudi na jinsi Daudi alivyoitikia ukosoaji huo.
Tazama 2 Samweli 11:1 – 12:25.

12. Rejelea matukio ya kale ya kukosolewa (Dakika 5-15)

Baadhi ya wanafunzi ni lazima wawe na mifano wazi (katika Mwongozo wa Somo Zoezi la 3) ya nyakati ambapo walirekebishwa au kukosolewa. Labda wengi wao watakubali kwamba hawakukubaliana na mtazamo wa kibiblia walipokuwa katika hali hiyo.

Huku ukitumia mifano ya Zoezi la 3, waeleze wanafunzi watafakari ni nini kingalitendeka kama wangetumia mtazamo wa Kibiblia walipokosolewa. Wanafunzi 2 au 3 watoe mifano yao.

Unaweza kuanza sehemu hii ya majadiliano kwa kutoa mifano ya maisha yako binafsi. Hili linaweza kukusaidia kuleta hali ya uwazi na ikawa rahisi kwao kuona unachokiangazia pale.

13. Jadili Hoja C: Je, kuna faida gani kutumia mtazamo wa kibiblia wakati ninarekebishwa au kukosolewa?
(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 24

Wanafunzi watoe orodha ya wanachokadiria kuwa manufaa ya kutumia huu mtazamo mpya.

Baada ya wao kutoa maoni yao, unaweza kuwaruhusu watazame maoni zaidi yaliyotwaliwa katika ukurasa wa 24 wa mwongozo wa mwanafunzi chini ya Hoja C *"Je, kuna faida gani kutumia mtazamo wa kibiblia wakati ninarekebishwa au kukosolewa?"*

Onyesha kwamba tabia zetu hubainisha mtazamo wetu halisi. Hauwezi kuitikia na kuwa na tabia mwafaka unapokosolewa isipokuwa uwe na mtazamo wa kibiblia.

14. Jadili Hoja D: "Je, ni matatizo yapi yanayohusiana na mtazamo huu?"
(Dakika 5-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 24-26

Pengine wanafunzi wako watapata urahisi wa kufanya orodha ya matatizo wanayokumbana nayo wanapojaribu kutumia huu mtazamo mpya wa kibiblia wanaporekebishwa au kukosolewa.

Waamuru waunde orodha ya matatizo yananyohusiana na mtazamo huu. Andika maoni yao kwa ubao au makaratasi makubwa na uyatundike ukutani. Waruhusu pia watoe vijisababu ni kwa nini mtazamo huo hautafua dafu.

Baada ya kutoa maoni yao, angalia orodha iliyotolewa katika ukurasa wa 24-26 katika Mwongozo wa Mwanafunzi tathmini kama utaongeza matatizo zaidi katika orodha yao.

Usihisi kushurutishwa kuhalalisha huu mtazamo wa kibiblia dhidi ya kila tatizo linaloorodheshwa.

2

Usikubali sehemu hii ya kipindi darasani kurundikwa na maoni hasi. Taja kwamba matatizo haya hayamaanishi kwamba mtazamo huu hauwezi kukuzwa. Matatizo haya yanaonyesha tu kwamba changamoto ni kubwa kwa wale kwa kweli wanataka kukuza mtazamo wa kibiblia ili kutumia wanapokosolewa.

15. Jadili Hoja E: Ninaanzaje kukuza mtazamo huu?
(Dakika 10-20) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 27

Wasilisha kwa wanafunzi hatua kadhaa tofauti wanazoweza kutumia kukuza mtazamo huu mpya katika maisha yao. Tumia nyenzo katika ukurasa wa 27 wa Mwongozo wa Mwanafunzi. Rejelea pia sura ya 2 ya Mwongozo wa Mwanafunzi ambapo inatoa hatua kadhaa za kukuza mtazamo mpya.

16. Jadili chati katika ukurasa wa 28-29 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi
(Dakika 5-15)

Kufikia hapa, unaweza kujadili chati kubwa kuhusu mtazamo huu iliyo kwa ukurasa wa 28-29 katika Mwongozo wa Mwanafunzi. Lenga majadaliano kwa safu ya nne au ya tano chini ya kichwa, “Niseme nini?”na “Nifanye nini?”

Eleza kwamba safu ya *“**Ubora Chanya wa Ndani**”* ni sehemu ya kukuza tabia kwa muda mrefu ambayo husaidia kuimarisha mtazamo mpya wanaokuza.

17. Dokezo la chaguo la kwanza katika somo la nne (4)

Huenda usipate muda wa kujadili kila wazo lililopo kwa somo hili kwa kipindi kimoja. Unwaeza kusibiri kujadili mengine katika somo la nne. (Tazama maagizo ya chaguo la kwanza kwenye mwongozo wa walimu kwa somo la nne, Mwongozo wa Mwalimu, ukurasa wa 34-37.)

Ikiwa utaamua kutumia Mbadala wa Kwanza kwwajili ya Somo la Nne, basi hakikisha umefunza Hoja E. *“Ninaanzaje kukuza mtazao huu?”*
(Sura 27 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.)

18. Kutendea somo kazi maishani (Dakika 5-10)

Kwa leo, lenga matumizi binafsi kwa kukuza mtazamo huu mpya wa kutumia unapokosolewa au kushutumiwa.

A. Eleza kwamba katika kipindi kijacho, watakuwa na mtihani kuhusu mawaza matano yanayounda mtazamo wa kibiblia ambao unatumika unapokosolewa au kushutumiwa.

B. Wahimize waanze kukariri maandiko yanayoambatana na kila mojawapo ya mtazamo. *Hawatatahiniwa kwa maandiko haya.*

C. Eleza kwamba Mwongozo wa Somo Zoezi la 4, *"Kuangalia Mara ya Pili Marekebisho na Ukosoaji wa Wakati Uliopita"* ni njia nyingine ya wao kuanza kukuza mtazamo huu.

D. Wahimize wawafafanulie viongozi na familia zao walichokisoma katika somo hili. Wahimize wapate usaidizi katika ukuzaji wa mtazamo huu mpya.

19. Kazi za somo

A. Baada ya kila kipindi cha darasa, uwape mtihani wa Methali 10:17.

B. Eleza jinsi Mwongozo wa Somo Zoezi la 4, *"Kuangalia Mara ya Pili Marekebisho na Ukosoaji wa Wakati Uliopita"* linaambatana na kazi yao kutoka kwa Zoezi la 3 *"Uzoefu Wangu wa Zamani wa Kurekebishwa au Kukosolewa."* Zoezi la 4 likamilishwe kabla ya somo la 4.

C. Sahihisha Zoezi la 2 Mwongozo wa Somo la leo kabla ya kipindi kijacho darasani.

20. Tathmini ya somo

Hebu andika mawazo yako kuhusu kuboresha hili somo.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

Somo la 3
Kuwarekebisha wengine

3

1. Kweli kuu ya Kibiblia

Ninapaswa kukariri na kutumia mtazamo wa Kibiblia ninapowakosoa wengine.

2. Mstari Mkuu: Wagalatia 6:1 (Biblia Habari Njema (SUV)

Ndugu, kama mkimwona mtu fulani amekosea, basi, nyinyi mnaoongozwa na Roho mwonyeni mtu huyo ajirekebishe; lakini fanyeni hivyo kwa upole, mkiwa na tahadhari msije nanyi wenyewe mkajaribiwa.

3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili

Sura ya 4 katika Mwongozo wa Mwanafunzi inaambatana na somo hili. Mazoezi ya 6-10 katika Mwongozo wa Somo pia yanaambatana na somo hili.

4. Zoezi la utangulizi wa somo: "Mchoro wa matofali" (Dakika 3-5)

Tanguliza somo hili kwa maelezo ya matofali.

Utahitaji:

1. Matofali mawili au matatu – aina ile ambayo hutumika kwa kujenga nyumba au mahali pa kuotea moto.

2. Kipande cha utepe na upinde wa kufungia kifurushi au zawadi.

3. Visanduku vidogo vya ukubwa wa tofali au kadibodi na utepe.

4. Kitabu chenye jalada gumu.

Matayarisho:

1. Funga tofali moja kwa kutumia utepe na upinde.
2. Kama hauna visanduku vidogo vya ukubwa wa matofali, basi viunde kwa kutumia kadibodi na utepe. Utahitaji angalau kadibodi 5 "matofali".
3. Kwa kutumia kalamu kubwa ya wino, andika vichwa vifuatavyo kwenye matofali ya kadibodi.

   --usivute sigara

   --usitamke matusi

   --wasamehe wengine

   --waheshimu viongozi

   --epuka vishawishi

   --usiseme uongo

4. Weka bahasha juu ya kitabu na uandike kichwa hiki juu yake, *Jinsi ya kujenga nyumba kwa matofali.*

Kuwasilisha kielelezo

Je, umewahi kugongwa na tofali? (Okota moja kati ya matofali). Watu wengine hupenda kuwatupia wenzao matofali. Njia mojawapo ambayo watu hukutupia matofali ni kwa kukushutumu. Hata japo mtu atajaribu kukukosoa kibiblia, bado hilo linauma. (Kufikia hapa, utamtupia mwanafunzi mmoja tofali lako la kadibodi)

Si mara nyingi mtu hukukosoa kwa njia ya upole. Wanakupa tofali lililofungwa kama zawadi, kisha wanasema, «Tumia hii, itakusaidia kuwa kama Kristo»
(Mpe mwanafunzi mmoja tofali lenye utepe na upinde.)

Katika kipindi kilichopita, tulisema kwamba kukosolewa kunaweza kukusaidia kusitawi. “Lakini”, unasema “ninasitawi vipi mtu anaponitupia tofali?”
Angalia mazingira yangu. Lazima kuwe na maelfu ya matofali amabayo yametapakaa. Kila ninapojaribu kufanya kitu, ninajikwaa kwenye matofali haya.

Kinachofanyika ni kwamba, watu hufanya kazi nzuri kutambua makosa yetu. Ifikiapo ni kutupa matofali, shabaha lao huwa aghalabu timilifu. Lakini ni nadra kwa anayekukosoa kuchukua muda kukusaidia kujenga kitu chenye manufaa kwa matofali anayokupa.

Unapomkosoa mtu aliyekosa, mpe zawadi mbili – tofali na usaidizi mdogo wa kutumia tofali hilo vyema. Mpe mwanafunzi mmoja tofali na kitabu chenye kichwa, Jinsi ya kujenga nyumba kwa motofali. Kisha jitolee kumsaidia mtu huyo kujenga tofali lako katika mtindo wa maisha yake ili wawe zaidi kama Kristo.

Kauli ya mpito:

Lengo kuu la somo la leo ni kuchunguza anachosema Mungu kuhusu jinsi ya kuwakosoa wengine.

5. Matukio yaliyopita ya kuwarekebishawengine (Dakika 5-10)

Ili kuwatayarisha wanafunzi kusikiliza somo la leo, unaweza kuwakubalia wachache kati yao kutoa mifano yao kutoka kwa Mwongozo wa Somo Zoezi la 7 *“Uzoefu Wangu wa Zamani wa Kurekebisha au Kukosoa Wengine”*.

Iwapo wanafunzi wanasita kutoa mifano yao, basi toa mifano yako kuhusu matukio ambayo umeyashuhudia hivi majuzi.

6. Jadili Hoja A: “Ninapaswa kumrekebisha nani?” (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 30-31

Pitia kwa ufupi swala la watu ambao wanafunzi wako wanapaswa kuwarekebisha. Jibu la swali hili linaweza kuwa tofauti sana kulingana na nani aliye darasani mwako. Taja kwamba kuwarekebisha wengine ni jukumu, wala sio uhuru.

A. Maswali mawili yanayohitaji uangalifu mkubwa.

- Unapaswa kuwarekebisha akina nani?
- Ni nani amekupa jukumu la kuwarekebisha wengine?

Maswali haya mawili ni muhimu sana katika kuweka msingi dhabiti kwa somo hili la leo. Iwapo wanadhani wako na uhuru wa kumrekebisha yeyote atendaye kosa, basi lipo tatizo.

3

B. Unda orodha ya watu wanaodhani wako na jukumu la kuwarekebisha.

Andika majibu yao kwenye ubao. Orodhesha watu hawa kwa upande mmoja.

C. Tambua ni nani amekupa jukumu la kuwarekebisha watu hawa.

Pitia orodha ya watu hawa tena na utambue ni nani amekupa jukumu la kuwarekebisha watu hawa.

Baadhi ya vyanzo viwezekanavyo vya jukuku hilo ni Mungu, wazazi, wachungaji, walimu shuleni, mnyapara kazini, mkurugenzi mkuu wa kampuni, askari, hakimu, sheria za nchi, jimbo au jiji, sharti lililowekwa na kikundi cha watu – klabu, kikosi nk.

Punde baada ya kufanya hivo, uliza swali:

D. Mtu huyu kweli alikuwa na mamlaka ya kukupa wewe jukumu hilo?

Ikiwa huyu mwenye mamlaka anatenda kwa cheo chake kwa ukweli, basi unaweza kumrekebisha mtu yule na kwa uhakika unatimiza wajibu wako. Sisitiza kwamba unahitajika kufanya hivyo daima na kwa upendo.

Taarifa zaidi kuhusu hoja hii imetolewa katika ukurasa wa 30-31 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

7. Masharti ya kuwarekebisha wengine kwa vijana.

Iwapo unafunza somo hili katika kituo cha vijana au huduma ya makazi sawia, ama hata gerezani, huu ndio wakati wa kujadili sheria ya mpango wako. Kama kituo chako hakina sheria au sera kuhusu hilo, basi unaweza kujadiliana na mkurugenzi wako ili uweze kuwapa wanafunzi jibu sahihi kuhusu majukumu yao.

Pia fafanua iwapo wana jukumu la kuwakosoa wafanyikazi au la.

Unaweza kutoa hali na kanuni tofautitofauti. Kwa mfano, tuseme kituo hakiwaruhusu wanafunzi kuwarekebisha wafanyikazi. Walakini, kama mfanyikazi anaendesha gari la wanafunzi na akose kuona hatari ya ajali ijayo, basi mwanafunzi anapaswa kuongea badala ya kupuuza hatari hiyo na kuacha ajali ifanyike.

8. Jadili Hoja B: "Ni mtazamo upi wa kibiblia tunapaswa kuwa nao tunapowarekebisha wengine?"
(Dakika 10-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 31-33

Unapoanzisha sehemu hii ya somo, eleza kwamba tutajadili mbinu tofauti za kuwarekebisha wengine baadaye. Kwa sasa tungependa kuzungumzia mawazo yaliyo akilini tunapojitayarisha kumkosoa aliyekosa.

Eleza uhitaji wa kutumia mtazamo wa kibiblia na mbinu yoyote ile tuitumiayo "kumpa mtu tofali"

Ni mtazamo upi wa kibiblia tunapaswa kuwa nao tunapowarekebisha wengine?

1. Mtu huyu ni mmoja wa marafiki speshieli wa Mungu.
   Ninataka kuwa na uwezo wa kutoa ripoti nzuri juu ya mtu huyu.
2. Mtu huyo alikosea nini?
3. Je, ni njia gani ya Mungu ya kurekebisha tatizo?
4. Ninawezaje kumsaidia mtu huyu kufuata njia ya Mungu?

Nukuu kutoka kwa Mitazamo mwongozo wa mwanafunzi ukurasa wa 31

3

9. Jadili Hoja C-1. "Mambo matatu ya kuzingatia unapochagua njia nzuri ya kumrekebisha mtu" (Dakika 5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 33-35

Hoja C, "Je, ni lazima niwarekebishe wengine?" Inaangazia baadhi ya mbinu zinazoweza kutumika kuwakosoa wengine.

Anza majadailiano yako ya mbinu za kuwakosoa wengine kwa kupitia hoja ndogo 1, "Mambo matatu ya kuzingatia unapochagua njia nzuri ya kumrekebisha mtu."

Kwa haraka zungumzia vigezo vitatu vya kuchagua mbinu mwafaka ya kumkosoa mtu. Jaribu kutoa vielezo kadhaa kufafanua kila mojawapo ya vigezo hivyo vitatu.

Mambo matatu ya kuzingatia unapochagua njia nzuri ya kumrekebisha mtu.

a. Ninamrekebisha nani?
b. Je, Jambo ambalo mtu huyo amefanya ni baya kwa kiasi gani?
c. Haiba yako itaathiri njia utakazotumia

Imenukuliwa kutoka kwa Mweongozo wa Mwanafunzi Ukurasa wa 33-35

10. Tanguliza hoja C-2. Mbinu za kibiblia za kuwarekebisha wengine (Dakika 5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa 35-38

Tumia sehemu kubwa ya kipindi darasani kujadili mbinu tofauti za kibiblia za kuwarekebisha wengine. Unapofanya utangulizi wa sehemu hii ya somo, taja kwamba kuna maandiko mengi yanayozungumzia kuwarekebisha wengine. Tunapaswa kuwa waangalifu tusichague andiko moja tu na kusema "Hii ndio mbinu ya kibiblia pekee, na mbinu hii ndio lazima itumike kila wakati." Mungu anaweza kutusaidia kuelewa ni mbinu gani zingine za kutumia katika hali tofauti. Maandiko matatu makuu yanatoa msingi kwa sehemu hii ya somo.

3

Wagalatia 6:1

Mathayo 18:15-17

2 Timotheo 3:16

Unapojadili kila mojawapo ya mbinu za kibiblia, waamuru wanafunzi wasome mandiko yaliyoorodheshwa kwa kila mbinu ya ukosoaji.

Wananafunzi watumie majibu yao kwa zoezi la 1,2 na 3 katika Mwongozo wa Somo Zoezi la 6, *"Mtazamo wa Kibiblia Kuhusu Kuwarekebisha Wengine."* Linganisha mbinu hizi na mawazo manne yaliyoorodheshwa katika ukurasa wa 31-33 katika Mwongozo wa Mwanafunzi, ambazo zinapaswa kujenga mtazamo wao wanapotumia kila mojawapo ya mbinu hizi.

Jaribu kuonyesha kutoka kwa maisha yako mwenyewe au kutumia mifano mingine ya kisasa jinsi kila moja ya njia hizi imetumika na vilevile matokeo yake.

11. Jadili Hoja C-2-a. Njia ya Wagalatia 6:1 ya kuwarekebisha wengine (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 35-36

Mwanzoni mwa mjadala wa mbinu ya Wagalatia 6:1 ya kuwarekebisha wengine, waulize wanafunzi kutambua ni nani anaambiwa akosoe. Maandiko haya yanasema watu wa kiroho ndio wanaopaswa kukosoa.

> **Wagalatia 6:1 (Biblia Habari Njema(SUV))**
>
> **Ndugu zangu, mtu akighafilika katika kosa lo lote, ninyi mlio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe.**

Waambie wanafunzi kwamba ikiwa wamekuwa Wakristo kwa majuma kadhaa, basi ingekuwa vema wasiwakosoe wengine, isipokuwa kama wamepewa jukumu maalum la kumrekebisha mtu huyu – kwa mfano – mwanake.

Mbinu ya Wagalatia 6:1 inaangazia hoja mbili kuu. Kwanza lengo letu linapaswa kuwa kumnadhifisha mtu huyu. Huku kunahusu zaidi ya kumwambia tu makosa aliyoyatenda. Hii ndiyo hatua yenye changamoto zaidi katika mchakato huu wa ukosoaji – na huweza kuwa na hatua nyingi zaidi, sio tu sekunde 60 za kukaripia.

Hoja ya pili lililoangaziwa hapa katika mbinu ya kuwarekebisha wengine ni kufanya hivyo kwa “upole”. Waulize wanafunzi watoe mifano ya vile wamekosolewa kwa upole. Kama hawapati mifano yoyote – huenda wakawa na matatizo kuiapata hapo mbeleni.

Unaweza kujadili jinsi inavyoweza kuwa chungu zaidi kwa yule anayekosolewa kuliko kwa mkosoaji. Unaweza kudhani kwamba unakosoa kwa upole, lakini mtu huyu mwingine anahisi vipi?

Kwa kuwa mpole, sisitiza umuhimu wa kuwa wazi. Kuwa mpole hakumaanishi kudokeza tu ya kwamba mtu ako na shida. Tunapaswa kuzungumza ukweli kwa upendo, lakini tuhakikishe kwamba tunaongea ukweli ili aelewe ya kwamba tunamkaripia kuhusu dhambi hiyo maishani mwake.

Jambo la mwisho lililotajwa hapa linastahili majadiliano, **“Lakini kuwa mwangalifu, la sivyo wewe pia unaweza kujaribiwa”.** Taja kwamba sio lazima tuwe wakamilifu ili tuwakosoe wengine, lakini lazima tujikinge. Yaani, dhambi katika maisha ya mtu mwingine yapaswa kuwa kengele ya kututahadharisha tulinde maisha yetu dhidi ya vishawishi vya mwovu shetani.

12. Jadili Hoja C-2-b. Njia ya Mathayo 18:15-17 ya kuwarekebisha wengine (Dakika 10-20) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 36

Mwambie mwanafunzi mmoja asome maandiko yanahusiana na mbinu hii ya ukosoaji. Taja kwamba mbinu hii ndio maarufu kabisa ya ukosoaji katika Bibilia.

Kwanza, wanafunzi watambue vizuizi vitatu vya matumizi ya mbinu hii.

1. Mtu huyo lazima awe Mkristo – Muumini.
2. Mtu huyo lazima awe ametenda dhambi – kuvunja amri moja ya Mungu.
3. Mtu huyo lazima awe amekukosea. Kama amemkosea mtu mwingine, basi mimi sina idhini ya kumkosoa, kulingana na maandiko haya.

Wanafunzi watambue hatua hizi tatu katika mbinu hii, na waziandike ubaoni au katika karatasi kubwa na waitundike kwenye ukuta wa darasa.

Mathayo 18:15-17 Biblia Habari Njema (SUV)

Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo. [16] La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike. [17] Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru.

Pitia kila hatua na ujadili kinachopaswa kufanywa. Taja kwamba katika hatua ya kwanza, mtu anapokuja kwako na kukuambia jinsi mtu mwingine alimkosea, unanpaswa kumwambia amrudie na amzungumzia pembeni, kulinga na maagizo ya Mathayo 18:15. Punde baada ya kufanya hivyo – na mtu yule akatae ule ukosoaji, basi utapanga kumwendea yule mtu wewe mwenywe.

Hakikisha ya kwamba sehemu hii ya kipindi ikite mizizi kwa ukweli – sio nadharia. Tumia mifano hususan kutoka maishani mwako, au maisha ya wengine karibu nawe. Usiingie kwa majadiliano ya kina kuhusu hali tatanishi zisizo na mzingi wa ukweli.

Watajie wanafunzi wako kwamba maandiko haya hayana vizuizi kuhusu hali yako ya kiroho kama sharti la kutumia mbinu hii. Hata ikiwa u Mkristo, mbinu hii ni sawa kwako wewe kutumia.

Sisitiza umuhimu wa kutumia maelekezo haya unapomkosoa mtu. Ikiwa watu wangezingatia mfumo wa Mathayo 18, ugomvi mwingi na kuvunjika kwa mahusiano kungezuiwa.

3

Wanafunzi watazame mifano yao katika Zoezi la 7 *"Uzoefu Wangu wa Zamani wa Kurekebisha au Kukosoa Wengine"* waone kama walimkosoa mtu pembeni ama kama palikuwapo watu wakati huo. Halafu, je, waliongea na watu wengine kuhusu shida hiyo kabla ya kumwambia huyu alitewakosea?

13. Jadili Hoja C-2-c. Njia ya 2 Timotheo 3:16 ya kuwarekebisha wengine (Dakika 10-20) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 36-38

Eleza mwanzoni kwamba 2 Timotheo 3:16 haizungumzii moja kwa moja jinsi watu wanavyopaswa kukosoana. Muktadha huu unajadili jinsi Biblia inavyoweza kutumika katika maisha ya Mkristo. Hata hivo, vigezo 4 muhimu vya maandiko haya vinatutolea misimamo mine ya kuwakosoa wengine.

2 Timotheo 3:16 Biblia Habari Njema (SUV)

Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki;

Baada ya mwanafunzi mmoja kusoma maandiko haya, andika orodha ya mbinu 4 zilizotolewa hapa na uzitundike ukutani mwa darasa. Jadili kila mbinu kivyake. Maelezo zaidi yametolewa kwenye mwongozo wa wanafunzi.

Unapozipitia mbinu hizi, taja kwamba zinaweza kutumika kibinafsi ama katika makundi. Baadhi ya mbinu hizi huenda zikaonekana zisizo za moja kwa moja kwa kumkosoa mtu. Ya kwanza – Funza ukweli – huenda hata ikakosa kumtambua mwenye makossa.

Jaribu kutoa mifano ya jinsi wewe au wengine wametumia mbinu hizi. Unaweza kuwauliza wanafunzi wabaini ni mbinu gani alizozitumia Yesu katika matukio haya.

a. Mtu aliyekuwa tajiri Mark 10:17-22

b. Mwalimu wa sheria Luka 10:25-38

c. Mwanamke mzinzi Yohane 8:1-11

d. Petro Mathayo 16:21-28

14. Jadili Hoja D: Je, ni mapendekezo yapi ya kuwakosoa wengine? (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 39-40

Kwa haraka pitia nyenzo zilizotolewa katkia mwongozo wa wanafunzi, zinazoangazia kila mojawapo wa hoja hizi. Katika hoja **ndogo 2, "Mwendee mtu huyo bila mapendeleo",** sisitiza umuhimu wa kuuliza maswali kama kipengee kikuu cha mbinu yoyote ya ukosoaji.

Katika kujadili hoja **ndogo 4, "Kuwa na mtazamo mzuri",** sisitiza ukweli ulioko katika Yakobo 1:19.

a. Kuwa hima kusikia

b. Usiwe mwepesi wa kusema

c. Usiwe mwepesi wa hasira

Chukua muda kujadili hoja **ndogo 6, "Je, na iwapo hawatakubali niwarekebishe?"** Hakikisha ya kwamba wanaona umuhimu wa kufanya kile Mungu anachokitaka wafanye , wala sio kuangalia tu jinsi anavyoitikia ukosoaji. Taja kwamba hatuwezi kumlazimisha mtu kukubali ukosoaji wetu.

15. Kuwarekebisha wengine na kuwasamehe wengine (Dakika 5-15)

Wanafunzi wajadili majibu yao ya swali la 4 na 5 katika Mwongozo wa Somo Zoezi la 6*"Mtazamo wa Kibiblia Kuhusu Kuwarekebisha Wengine."*

(4) Je, Yesu alisema nini juu ya kuwasamehe wale wanaokutenda dhambi? (Mathayo 18:15-22)

(5) Ni nini maoni yako. Je, unapaswa kumsamehe Mkristo hata kama yeye atakataa kusikiliza wakati unapojaribu kumrekebisha? Eleza jibu lako.

Maswali haya mawili yanaibua hoja muhimu sana kuhusu mchakato wa kuwaokosoa wengine. Hata kama mwanafunzi anafuata maelekezo ya Biblia wakati wa kumkosoa mtu, mtu huyo baado anaweza kuitikia kwa njia ya kukera.

Mwanafunzi wako asifikirie kwamba kutumia mitazamo ya Kibiblia na mbinu hizi kutamuhakikishia kuwepo kwa mazungumzo ya Amani na fanaka. Lazima wawe tayari kukabiliana na hasira na kutupiwa maneno makali wanapojaribu kutenda wema.

Maana ya msamaha wa kweli itadhihirika hivi karibuni wakati utakapokumbana na hali kama hizi. Taja kwamba lazima tutumie mitazamo ya kibiblia tunapowakosoa wengine na kuitikia kwa msamaha hata waitikie kwa njia yoyote ile.

16. Jadili Hoja E: Je, ni vizuizi vipi vya Kibbilia vya kuwarekebisha wengine? (Dakika 10-20) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 40-43

Pitia kwa haraka hoja ndogo zilizotolewa katika sehemu hii ya Mwongozo wa Mwanafunzi. Panga muda kwa kila hoja kulingana hali ya wanafunzi katika darasa lako.

Kama bado hamjajadili swala la **"Je, ninapaswa kuwarekebisha viongozi wangu?"** basi chukua muda hapa (**Hoja ndogo 6**) kuhakikisha kuwa wanaelewa jinsi ya kulikabili swala hili. Jambo moja unalopaswa kuibua ni matokeo ya kuwakosoa viongozi wako. Ukimkosoa mkubwa wako kazini, unaweza ukapigwa kalamu. Unapaswa kuangalia madhara kabla ya kuwakosa wakubwa wako. Haimaanishi kwamba hatufai kuwakosoa viongozi.

Wanafunzi wajadili majibu yao kwa mfano halisi kutoka kwa Mwongozo wa Somo Zoezi la 6 (swalo 6)

"Terri afanye nini? Eleza kwanini."

3

17. Kutendea somo kazi maishani (Dakika 5-10)

Kwa matumizi binafsi leo, wanafunnzi wafanye mambo matatu.

A. Wahimize wakariri mawazo manne (4) yaliyowekwa katika mtazamo wa kibiblia wa kutumia tunapowakosoa wengine. Tazama ukurasa wa 31-33 katika Mwongozo wa Mwanafunzi kwa maelezo zaidi.

Ni mtazamo upi wa kibiblia tunapaswa kuwa nao tunapowarekebisha wengine?

1. Mtu huyu ni mmoja wa marafiki speshieli wa Mungu.
   Ninataka kuwa na uwezo wa kutoa ripoti nzuri juu ya mtu huyu.
2. Mtu huyo alikosea nini?
3. Je, ni njia gani ya Mungu ya kurekebisha tatizo?
4. Ninawezaje kumsaidia mtu huyu kufuata njia ya Mungu?

Nukuu kutoka kwa Mitazamo mwongozo wa mwanafunzi ukurasa wa 31

B. Waache wabuni kumbukumbu itakayowasaidia.

Mpe kila mwanafunzi kadi. Waagize waandike mitazamo ya kibiblia watakayotumia kuwakosoa wengine. Wape kalamu za wino na za rangi watumie kunakshi kadi zao wanavyotaka.

Pia waandike katika kadi hizi maoni mengine makuu wanayohitajika kukumbuka wanapomkosoa mtu. Kwa mfano, wangependelea kuandika mojawapo ya maandiko yaliyojadiliwa leo. Wakikamilisha kuandika kwa kadi zao, wahimize wazitundike katika chumba au kuzitumia kama alamisho.

C. Tamatisha kipindi cha leo kwa sala ya uwajibikaji.

Wahimize wanafunzi kufanya ahadi na Mungu ya kuanza kutumia mitazamo ya kibiblia na mbinu za kibiblia wanapowakosoa wengine.

18. Kazi za somo

A. Sahihisha Mwongozo wa Somo Zoezi la 2, 4, 6 na 7.

B. Eleza jinsi Mwongozo wa Somo Zoezi la 8 unaambatana na kzi waliyoifanya katika Zoezi la 7. Taja kwamba lengo la zoezi hili ni kuwasaidia kuona jinsi wanavyoweza kutumia mitazamo ya Kibiblia kuwakosoa wengine.

C. Mwishoni mwa kipindi, toa mtihani kuhusu Wagalatia 6:1.

D. Aidha leo ama katika kipindi kifuatacho, wape mtihani kuhusu mawazo yanayohusishwa katika mtazamo wa kibiblia utakaotumika katika ukosoaji. Wanapaswa kuandika kutoka kwa kumbukumbu na katika mpangilio mwafaka yale mawazo yanayohusishwa katika mtazamo huu, na alama za ziada wanaponukuu maandiko yanayoandamana na kila hatua.

Mtazamo wa kibiblia unaofaa wakati wewe unasahihishwa au unakosolewa

1. Ninarekebishwa (au kukosolewa). Mithali 10:17
2. Nitasikiliza kwa makini. Yakobo 1:19
3. Ninashukuru kwamba ananirekebisha. 1 Wathesalonike 5:18
4. Nilikosea. Mithali 28:13
5. Ninawezaje kuzuia jambo hili baya kutokea tena? Mithali 15:31-32

Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi Ukurasa wa 15

E. Eleza kwamba Mwongozo wa Somo Zoezi la 9, *"Kutumia Mtazamo Wangu Mpya Wakati Ninamsahihisha Mtu"* si lazima. Hawapaswi kuukamilisha kabla ya mwisho wa kozi hii.

F. Ukichukua chaguo 2 katika somo la Nne (4) basi itakubidi kukamilisha zoezi fupi litakalowatayarisha kwa kipindi cha darasa.

Tengeneza zoezi ili walilete wakati wa kipindi kifuatacho cha darasa. Waagize waeleze mifano miwili au mitatu inayoonyesha mtazamo kwa hoja mahsusi unalopanga kujadili. Unaweza kuitengeneza kwa muundo sawia na uke wa Zoezi la 3 na Zoezi 7.

19. Tathmini ya somo

Hebu andika mawazo yako kuhusu kuboresha hili somo.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

Somo la 4
Utangulizi wa jumla

1. Uko na chaguo mbili za kufikiria katika mpangilio wa kipindi cha leo.

Chaguo 1: Tumia kipindi hiki kwa mitazamo ile miwili iliyowasilishwa katika somo la 2 na 3

"Mtazamo wangu ninapokosolewa"

"Mtazamo wangu ninapowakosoa wengine"

Chaguo 2: Tumia kipindi hiki kukabiliana na moja au zaidi ya mitazamo unayohisi itakuwa yenye manufaa katika darasa. Tazama ukurasa wa 38, kipengee 3, katika Mwongozo wa Mwalimu upate mada zilizopendekezwa kwa kipindi hiki.

Chaguo zote mbili zimejadiliwa kwa kina katika kurasa zifuatazo.

4

2. Marejeleo ya mwanafunzi

Creative Bible Teaching, na Larry Richards (Moody Press). Sura ya 9-16 ziko na maoni mazuri ya jinsi ya kupanga somo. Pengine maoni haya yatakuwa ya manufaa kwako katika kupanga somo la leo.

3. Kweli kuu ya Kibiblia

Kweli kuu ya kibiblia hii leo italingana na utakachochagua kufunza. Ukichukua **chaguo 1**, "Mtazamo wangu ninapokosolewa" na/ama "Mtazamo wangu ninapowakosoa wengine", utatumia ukweli halisi wa kibiblia kutoka kwa masomo hayo mawili

Ukichukua **chaguo 2**, basi utahitajika kuandika ukweli wako halisi wa kibiblia. Lengo la ukweli wa kibiblia ni kufupisha hadi sentensi moja lengo kuu la kipindi cha darasani.

4. Mstari mkuu wa Somo hili

Ukichukua **chaguo 1**, maandiko makuu ya leo yanaweza kuwa sawia na yale ya somo la 2 na/ama 3.

Ukichukua **chaguo 2**, jaribu upate aandiko linalohusiana na maswala unayotaka kupitia katika somo hili.

Somo la 4
Chaguo la 1

Mtazamo wangu ninapokosolewa

Mtazamo wangu ninapowakosoa wengine

1. **Kweli Kuu ya Kibiblia:** Sawia na somo la 2 na/ama 3

_____

_____

_____

2. **Mstari Mkuu:** Sawia na somo la 2 na/ama 3

_____

_____

_____

3. **Taja mikakati yako ya somo**

Hakikisha kwamba uko na maoni bayana kuhusu unachotaka kujadili katika darasa la leo. Unaweza kuchukua muda ili kujadili maswali au matatizo waliyo nayo wanafunzi katika matumizi ya mitazamo hii miwili. Kuwa tayari na mipangilio yako iwapo hawatukuwa na maswali.

4. **Matumizi ya mifano halisi**

Inaweza kuwa na manufaa iwapo utajadili mifano halisi ya matukio pale ambapo watu waliitumia mitazamo hii. Mifano yao kutoka kwa Mwongozo wa Somo, Zoezi la 3 na 7 inaweza kusaidia sana hapa. Waulize watambue mitazamo waliyokuwa nayo watu wote wawili. Je, yanakaribiana na mfumo wa kibiblia? Wangewezaje kuzingatia biblia zaidi katika kuitika kwao?

5. **Matumizi ya vichekeso na maigizo mafupi**

Wanafunzi waigize tukio ambalo mmoja anamkosoa mwingine. Wayatamke mawazo yao. Kitabu cha Marlene D. LeFever *Creative Teaching Methods* (David C. Cook Publisher) kina sura mwafaka ya jinsi ya kutumia maigizo darasani.

Nyenzo nyingine nzuri inayofafanua matumizi ya vichekesho na maigizo mafupi ni *How to Do Bible Learning Activities*, by Ed Stewart & Neal McBride (Gospel Light Pub.). Yanapatikana matoleo mawili ya kitabu 1 – moja ni kwa watu wazima na lingine

kwa darasa la 7-12. Buku 2 na kwa kichwa sawia pia yapatikana kwa darasa la 7-12 tu. (na Rich Bundschuh and Annette Parrish).

Andika sehemu ambazo waigizaji watacheza ili waweze kuzijua (na pia wewe ujue) nini cha kufanya.

Wakati wanafunzi wako wanapofanya hili darasani, hebu kuwe na mtu wa kuwanasa kwenye video. Wanafunzi watafurahi kujiona baadaye wakiigiza, na kila mara wakiona video hiyo itakuwa fursa ya kutilia mkzao yale umekuwa ukiwafunza katika somo hili.

6. Matumizi ya Maandiko

Unaweza kutumia sehemu ya kipindi cha darasa kujadili maandiko yanayohusiana na mitazamo hii. Ingekuwa vyema kama ungetayarisha orodha ya maandiko kabla ya kipindi kuanza. Unaweza kuwaagiza wanafunzi waangalie maandiko na kutathmini jinsi yanavyohusiana na mitazamo hii.

Mnaweza kufanya hili kwa pamoja au wafanye kwa vikundi vidogovidogo na kutungu orodha ya maandiko. Wape makaratasi makubwa na kalamu kubwa za wino kuandika uvumbuzi wao. Kisha mbele ya darasa, kila kikundi kiwasilishe ripoti kilichopata.

Mwongozo wa Somo, Zoezi la 10 *"Hekima ya Kibiblia na Marekebisho"* unaweza kutumika vizuri hapa.

7. Kutendea somo kazi maishani (Dakika 5-10)

Maliza kipindi cha somo kwa matumizi binafsi yanayofaa. Kwa vidokezo, tazama nyuma kwa matumizi binafsi ya mazoezi yaliyotolewa katika vipindi viwili vilivyopita.

_____

_____

_____

_____

8. Kazi za somo

A. Sahihisha Mwongozo wa Somo, Zoezi la 4 kama bado haujafanya hivo.

B. Sahihisha Mwongozo wa Somo, Zoezi la 5 aidha leo ama katika kipindi kijacho.

C. Waeleze wanafunzi wako kwamba wanapaswa kuwa wamekamilisha Mwongozo wa Somo, Zoezi la 8 kabala ya kipindi kifuatacho – hiki ndicho kipindi cha mtihani kwa kozi hii.

D. Baada ya kipindi hiki, toa mjarabu kuhusu *"Mtazamo wa kibiblia unaofaa wakati unasahihishwa au kukosolewa"* kama haukua umefanya hivyo katika kipindi kilichopita.

Mtazamo wa kibiblia unaofaa wakati wewe unasahihishwa au unakosolewa

1. Ninarekebishwa (au kukosolewa). Mithali 10:17
2. Nitasikiliza kwa makini. Yakobo 1:19
3. Ninashukuru kwamba ananirekebisha. 1 Wathesalonike 5:18
4. Nilikosea. Mithali 28:13
5. Ninawezaje kuzuia jambo hili baya kutokea tena? Mithali 15:31-32

Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi Ukurasa wa 15

9. Tathmini ya mwalimu kwa kipindi cha darasa la leo

Baada ya kumaliza kipindi, andika tathmini fupi ya darasa la leo.
Tafadhali orodhesha maoni yako ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu gani ziliokuwa bora zaidi?
Ni sehemu gani zilizokuwa ngumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni nini kilichokuwa cha manufaa kwa wanafunzi wako?

Somo la 4
Chaguo la 2

Mtazamo wa chaguo lako

1. Kweli Kuu ya KiBiblia

_____

_____

_____

4

2. Mstari Mkuu

_____

_____

_____

3. Upangaji wa mikakati yako

Utumie muda wa kipindi hiki kuangazia mtazamo mmoja au zaidi unaofikiria utakuwa wenye manufa katika darasa. Kurasa 7 wa Mwongozo wa Mwanafunzi zimetoa orodha ya mitazamo ambayo wakristu wapya wameonyesha ari ya kusoma. Mwongozo wa Somo, Zoezi la 1 na 2 yote yana maswali ambayo yanakupa mawazo yenye manufaa kuhusu wanachotaka kusoma wanafunzi wako.

Hizi ni baadhi ya mada zilizopendekezwa kwa kipindi hiki cha darasa.

- Vishawishi vya kutenda dhambi, kwa mfano, uchu
- Hadhi binafsi – mtazamo wako mwenyewe kwa nafsi yako
- Hasira
- Mahusiano na watu wengine

_____

_____

_____

_____

4. Jua mapendezo ya wanafunzi wako

Ukitaka wanafunzi washiriki kikamilifu katika maamuzi ya mitazamo ya kusoma, pata maoni yao kabla ya kipindii cha leo. Hii ni muhimu haswa ikiwa utataka kuwapa kazi ya ziada inayohusiana na mtazamo utakao kuwa unawasomesha. Tazama maagizo mwishoni mwa mpangilio wa somo la 3 kwa kazi ya ziada ambayo wanapaswa kukamilisha kabla ya kipindi cha leo (Hoja 18-F, Mowongozo wa Mwalimu, ukurasa wa 33)

5. Jinsi ya kukuza mtazamo mpya

Unaweza kutumia sehemu ya maarifa kutoka kwa Sura ya 2 katika Mwongozo wa Mwanafunzi kupanga somo la leo. Wanafunzi walinganishe vidokezo vya jinsi ya kukuza mtazamo mpya na mada ulioichagua katika kwa kipindi cha leo.

6. Shabaha lako litakuwa nini katika darasa la leo?

Utahitajika kuamua ni kiasi kipi cha muda wa kipindi cha darasani kitengwe kwa kila mojawapo wa mada zifuatazo:

a. Kujenga ufahamu wa mitazamo yao ya sasa katika eneo hili.

b. Wataanzia wapi kukuza mtazamo mpya katika sehemu hii ya maisha.

7. Matumizi ya maandiko

Kuwa na orodha ya maandiko yanayogusia mtazamo huo. Wagundue na kufafanua jinsi kila andiko linavyohusiana na mtazamo huu.

8. Ni mawazo yapi yatakayounda mtazamo huu mpya?

Kisha, watoe orodha ya mawazo makuu yatakayotiwa katika mtazamo mpya tunaotaka kukuza. Unaweza kuunda kitu sawia na kile kilichofanywa katika mitazamo iliyojadiliwa katika Sura ya 3 na 4 katika mwongozo wa wanafunzi. Jaribu uwe na maadiko yanayoambatana na kila hoja.

Ili kujadili matumizi halisi ya mtazamo huu, tumia baadhi ya mifano kutoka kwa kazi ya ziada uliyowapa.

9. Kutendea somo kazi maishani (Dakika 5-10)

Buni matumizi binafsi ifaayo kwa somo hilo. Angazia uhitaji sio wa kukariri mfumo mpya wa fikira bali pia wajumuize kuanza kuzitumia katika matukio yanayowakumba juma hili.

_____

_____

_____

10. Kazi za somo

A. Sahihisha zoezi lao maalum la kipindi cha leo.

B. Sahihisha Mwongozo wa Somo, Zoezi la 4 kama bado haujafanya hivo.

C. Sahihisha Mwongozo wa Somo, Zoezi la 5 aidha leo ama katika kipindi kifuatacho.

D. Waeleze wanafunzi wako kwamba wanapaswa kuwa wamekamilisha Mwongozo wa Somo, Zoezi la 8 kabla ya kipindi kifuatacho – hiki ndicho kipindi cha mtihani kwa kozi hii.

E. Baada ya kipindi hiki, toa mjarabu kuhusu *"Mtazamo wa kibiblia unaofaa wakati unasahihishwa au kukosolewa"* kama haukua umefanya hivyo katika kipindi kilichopita.

4

Mtazamo wa kibiblia unaofaa wakati wewe unasahihishwa au unakosolewa

1. Ninarekebishwa (au kukosolewa). Mithali 10:17
2. Nitasikiliza kwa makini. Yakobo 1:19
3. Ninashukuru kwamba ananirekebisha. 1 Wathesalonike 5:18
4. Nilikosea. Mithali 28:13
5. Ninawezaje kuzuia jambo hili baya kutokea tena? Mithali 15:31-32

Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi Ukurasa wa 15

11. Tathmini ya mwalimu kwa kipindi cha darasa la leo

Baada ya kumaliza kipindi, andika tathmini fupi ya darasa la leo.
Tafadhali orodhesha maoni yako ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu gani ziliokuwa bora zaidi?
Ni sehemu gani zilizokuwa ngumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni nini kilichokuwa cha manufaa kwa wanafunzi wako?

Somo la 5
Mtihani

1. Utangulizi

Fanya utangulizi wa somo litakalofuata.

A. Wape Mwongozo wa Somo au Mazoezi yoyote ambayo yanapaswa kukamilishwa kabla ya kipindi cha kwanza cha kozi ifuatayo utakayofundisha.

B. Waelekeze wanafunzi kufungua ukurasa wa mwisho katika Mwongozo wa Somo Lipya. Wanapaswa kupata nakala safi ya ***Orodha ya Kazi za Darasani.***
Wape tarehe za majaribio ya chemsha bongo, Zoezi, na mtihani.

C. Wape Mwongozo wa Mwanafunzi mpya na uwaambie kurasa watakazosoma kabla ya kipindi kifuatacho darasani.

2. Wape mtihani wa Somo hili.

3. Ikiwa hujafanya hivyo bado, rudisha chemsha bongo zote na mazoezi ambayo umesahihisha.

Kwa kozi hii ya ***Mitazamo,*** Mwongozo wa Somo, Zoezi la 5, 8, 9 na 10 huenda ikawa zilipangwa kutwaaliwa leo.

Mwongozo wa Mwanafunzi

Mwongozo wa Mwanafunzi Haujajumuishwa kwenye hati hii,
lakini unapatikana katika hati tofauti.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Mwanafunzi.

Mwongozo wa Somo

Haukujumuishwa kwenye hati hii, lakini unapatikana katika hati tofauti.

.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Somo.

Mtihani

Majibu ya mtihani

Cheti cha Somo

Tazama ukurasa wa 5 wa mwongozo huu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mtihani na cheti.

Jina_____ **Mitazamo**

Tarehe_____ **Mtihani wa Toleo la 5**

Darasa_____ _____**Alama**

Maswali ya Kweli au Si Kweli (Alama 1 kwa kila swali)

Maelekezo: Weka alama ya ____X____ ikiwa jibu ni kweli.

Weka alama ya ____O____ ikiwa jibu si kweli.

1. _____Mtazamo ni sawa na hisia.

2. _____Mitazamo ambayo Yesu alikuwa nayo ndiyo aina bora ya kutumia ikiwa unataka kuwa Mkristo aliyefanikiwa.

3. _____Watu hutumia tu mitazamo wanapokasirika juu ya jambo fulani.

4. _____Wakati ninasahihishwa, ninapaswa kusikiliza kwa uangalifu, isipokuwa ninajua nilikuwa sahihi.

5. _____Ikiwa unajua mtu amefanya jambo baya, unapaswa kumsahihisha mtu huyo hata kama ulikuwa sehemu ya shida.

6. _____Mtazamo ni jinsi unavyofikiria juu ya jambo fulani.

7. _____Kuota ndoto za mchana kunaweza kuwa njia bora ya kukuza mitazamo ya Kibiblia.

8. _____Wakati mtu ana tabia mbaya, kawaida ni kosa la mtu mwingine.

9. _____Mitazamo ya mtu ina ushawishi mdogo sana kwa shughuli zake za kila siku na jinsi anavyojibu katika hali hizi.

10. _____Hakuna kitu mtu anaweza kufanya kubadili mitazamo ambayo alifundishwa kama mtoto mdogo.

11. _____Njia ya pekee ambayo mtu anaonyesha mitazamo yake ni kwa yale anayosema.

12. _____Mtu anapoanza kukurekebisha, jambo la kwanza unalopaswa kufanya ni kumtaka naye asikilize upande wako wa hadithi.

13. _____Ni bora kujibu kwa hasira kuliko huzuni wakati mtu anakurekebisha.

14. _____Mtu anapokurekebisha kwa njia isiyofaa, unapaswa kuwaambia mara moja ni nini wanakosea.

15. _____Kila wakati unasahihisha mtu, lazima umwambie kile alichokosea.

Maswali Mafupi

1. Orodhesha faida tatu za kutumia mtazamo wa kibiblia wakati unasahihishwa.
(Alama 9, kila sehemu alama 3)

A._____

B._____

C._____

2. Mtazamo ni nini? (Alama 4)

_____

_____

_____

3. Je, mtu huonyeshaje mitazamo yake? Orodhesha njia tatu.
(Alama 6, kila sehemu alama 2)

A._____

B._____

C._____

4. Je, ni mtazamo gani wa kibiblia wa kutumia tunaposahihishwa? Orodhesha mawazo 5 ambayo yanaunda mtazamo wa kibiblia uliowasilishwa katika kozi hii.
(Alama 10, kila sehemu alama 2)

A._____

B._____

C._____

D._____

E._____

5. Je, ni mtazamo gani wa kibiblia wa kutumia unapomsahihisha mtu? Orodhesha mawazo manne ambayo yanaunda mtazamo wa kibiblia uliowasilishwa katika kozi hii.
(Alama 8, kila sehemu alama 2)

A._____

B._____

C._____

D._____

6. Mathayo 18:15-17 inatoa hatua tatu za kutumia wakati wa kusahihisha Mkristo aliyefanya jambo baya. Eleza ni nini unapaswa kufanya katika kila hatua ikiwa unasahihisha mtu. (Alama 12, kila hatua alama 4)

   A. _____

   _____

   _____

   _____

   B. _____

   _____

   _____

   _____

   C. _____

   _____

   _____

   _____

7. Andika mistari ya kukariri hapa chini. (Alama 12, kila mstari alama 6)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Kisa cha Kujifunza

Lakesha amekasirika. Pam alimuaibisha tu mbele ya darasa nzima la somo la historia. Lakesha anamngojea Pam nje kidogo ya mlango wa darasa. “Je, unafikiri wewe ni nani, kuwaita watu wangu watumwa wajinga?” anasema Lakesha. “Ninyi nyote ni takataka nyeupe.” Lakesha anaondoka huku Pam na marafiki zake wakimcheka.

Ulikuwa katika darasa la historia na kusikia kile Pam alisema darasani. Uliona pia majibu ya hasira ya Lakesha baada ya darasa. Wote Lakesha na Pam wanahudhuria kanisa lako na wanasema ni Wakristo.

1. Unaamua kuzungumza na Pam na unajaribu kumsahihisha.

   A. Je, unafikiri Pam alifanya makosa gani? (Alama 2)

   _____

   _____

   B. Kulingana na yale uliyojifunza wiki hii juu ya kumsahihisha mtu, ungemwambia nini Pam? (Alama 10)

   _____

   _____

   _____

   _____

   _____

   _____

2. Unaamua pia kuzungumza na Lakesha na ujaribu kumsahihisha.

   A. Unafikiri Lakesha alifanya nini ambacho kilikuwa kibaya? (Alama 2)

   _____

   _____

   _____

   _____

   B. Kulingana na yale uliyojifunza wiki hii juu ya kusahihisha mtu, ungemwambia nini Lakesha? (Alama 10)

   _____

   _____

   _____

   _____

   _____

   _____

Mitazamo

Mtihani wa Toleo la 5

Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

Ukurasa wa 1

Maswali ya Kweli au Si Kweli

(Alama 1 kila moja)

1. 0 Si kweli
2. X Kweli
3. 0 Si kweli
4. 0 Si kweli
5. 0 Si kweli
6. X Kweli
7. X Kweli
8. 0 Si kweli
9. 0 Si kweli
10. 0 Si kweli
11. 0 Si kweli
12. 0 Si kweli
13. 0 Si kweli
14. 0 Si kweli
15. 0 Si kweli

Mitazamo

Mtihani wa Toleo la 5

Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

Ukurasa wa 2

Maswali Mafupi

(Majibu yaliyopendekezwa hayahitaji maneno halisi yaliyoorodheshwa hapa chini kuwa sahihi.)

1. Alama 9, alama 3 kila sehemu
   Majibu yanayopendekezwa:

   A. Unazuia shida nyingi
   B. Unamfurahisha Mungu
   C. Unaweza kubadilisha uzoefu unaoumiza na ukawa fursa ya ukuaji
   D. Unaweza kujenga urafiki thabiti

2. Alama 4
   Majibu yanayopendekezwa:

   A. Mfano wa kufikiria
   B. Maoni
   C. Njia unayofikiria juu ya jambo fulani
   D. Tabia ya kufikiria
   E. Maoni
   F. Mawazo ambayo nimejifunza
   G. Msimamo wa kiakili kuhusu ukweli au hali

3. Alama 6, alama 2 kila sehemu
   Majibu yanayopendekezwa:

   A. Kwa kile anachosema
   B. Kwa kile anachofanya
   C. Toni ya sauti yako

4. Alama 10, alama 2 kila sehemu
   Majibu yanayopendekezwa:

   1. Ninarekebishwa.
   2. Nitasikiliza kwa makini.
   3. Ninashukuru kwamba ananirekebisha.
   4. Nilikosea.
   5. Ninawezaje kuzuia jambo hili baya kutokea tena?

5. Alama 8, alama 2 kila sehemu
   Majibu yanayopendekezwa:

   A. Mtu huyu ni mmoja wa marafiki speshieli wa Mungu. Ninataka kuwa na uwezo wa kutoa ripoti nzuri juu ya mtu huyu.
   B. Mtu huyo alikosea nini?
   C. Je, ni njia gani ya Mungu ya kurekebisha tatizo?
   D. Ninawezaje kumsaidia mtu huyu kufuata njia ya Mungu?

Mitazamo

Mtihani wa Toleo la 5

Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

Ukurasa wa 3

6. Alama 12, alama 4 kila sehemu
   Wanafunzi wanaweza kuweka hii kwa maneno yao wenyewe.

   A. Mathayo 18:15 (Bibilia Takatifu SUV) Na ndugu yako akikukosea, nenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo

   B. Mathayo 18:16 (Biblia Takatifu SUV) La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike.

   C. Mathayo 18:17 (Biblia Takatifu SUV) Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru.

7. Aya za kukariri
   Alama 12, alama 6 kila kifungu

   Mithali 10:17

   Wagalatia 6:1

Ukurasa wa 4

Kisa cha Kujifunza:

Majibu yaliyoorodheshwa hapa chini ni majibu yote yaliyopendekezwa

1. A. (Alama 2)

   Pam alikosea kusema kwamba watu kama Lakesha walikuwa watumwa wasiojua. Alikosea jinsi alivyojibu wakati alijua kwamba alikuwa amemuumiza Lakesha

   B. (Alama 10)

   Jibu lao linapaswa kuendana na mojawapo wa njia za marekebisho zilizojadiliwa katika kozi hii.

2. A. (Alama 2)

   Lakesha alikosea kumrekebisha Pam hadharani, haswa mbele ya marafiki zake. Lakesha alikosea kumwita Pam “takataka nyeupe.”

   B. (Alama 10)

   Jibu lao linapaswa kuendana na mojawapo wa njia za marekebisho zilizojadiliwa katika kozi hii.

Hongera

_____

Amemaliza

Mitazamo

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya
na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio utaendelea
na masomo yako yajayo.

Wakufunzi _____

Tarehe _____

Hongera

_____

Amemaliza

Mitazamo

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya
na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio utaendelea
na masomo yako yajayo.

Wakufunzi _____

Tarehe _____